TOLEO LA 47
NA. 00000394

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA MAKAMU WA RAIS

JARIDA LA
**AGOSTI 2025**



# HOJA 15 ZA MUUNGANO ZIMEPATIWA UFUMBUZI AWAMU YA SITA

#MUUNGANO WETU
#UMOJA WETU

#MAZINGIRA YETU,
#UHAI WETU



**IKOLOJIA BAHARI:** DKT. MPANGO AHIMIZA USIMAMIZI



**FURSA KABONI;** WAWEKEZAJI WAFUNGUA MILANGO



**NISHATI SAFI YA KUPIKIA YAHIMIZWA**

# MUUNGANO WETU;

## Hoja 15 za Muungano zimepatiwa ufumbuzi Awamu ya Sita



**Serikali ya Awamu ya Sita kati ya kipindi cha mwaka 2021-2025 imezipatia ufumbuzi hoja 15 za masuala ya Muungano.**

Akihutubia katika mkutano wa kuhitimisha shughuli za Bunge la 12 jijini Dodoma Juni 27, 2025, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema utatuzi wa hoja hizo umezidi kuongeza imani ya Watanzania kwa Serikali.




"Nilipokabidhiwa dhamana ya kuiongoza nchi yetu, niliahidi kudumisha Tunu za Taifa letu yaani amani, umoja na mshikamano, uhuru wa nchi yetu, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar pamoja na kudumisha Muungano wetu," **amesema Rais Samia**.

Rais Samia ameongeza kuwa kama ilivyokuwa kwa Serikali za Awamu zilizopita, Tanzania imeendelea kujivunia tunu za amani, umoja na mshikamano ambazo zimeendelea kuimarika siku hadi siku na kuwafanya Watanzania kuendelea kuwa wamoja.

Amesema yapo mashirikiano licha ya Watanzania kuwa na tofauti zao za kidini, mila na desturi, itikadi za kisiasa na hata ushabiki wa michezo, na kuwaasa kushikamana na kuwa makini na vitisho vyovyote dhidi ya Muungano.

"Nafurahi kuwataarifu kwamba maagizo yangu yale yametekelezwa kwa ufanisi zaidi chini ya uenyekiti wa Makamu wa Rais akisaidiwa na Waziri Mkuu kwa upande wa Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar Makamu wa Pili wa Rais," alisema Rais Samia na kuwahimiza kuendeleza umoja, utulivu na amani vitu ambavyo ni sifa njema kwa taifa, alisema Dkt. Samia.

> Nilipokabidhiwa dhamana ya kuiongoza nchi yetu, niliahidi kudumisha Tunu za Taifa letu yaani amani, umoja na mshikamano, uhuru wa nchi yetu, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar pamoja na kudumisha Muungano wetu
>
> Mhe.Dkt.Samia Suluhu Hassan
> Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# DKT. MPANGO: VIONGOZI TUKABILI MABADILIKO YA TABIANCHI

> Matumizi bora ya rasilimali, uwekezaji katika nishati mbadala na teknolojia rahisi na nafuu,
>
> **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango**
> Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango amesema viongozi wa taasisi na mashirika wanawajibika kuchangia juhudi za Serikali katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuandaa na kutekeleza mikakati ya kupunguza uzalishaji wa gesijoto na kuhimili athari za mabadiliko hayo.

Makamu wa Rais amesema hayo wakati akifungua Mkutano wa Viongozi wa Taasisi na Mashirika ya Umma kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na Biashara ya Kaboni uliofanyika katika Ukumbi wa APC – **Mbweni jijini Dar es Salaam Machi 6, 2025.**

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesema mikakati itakayoandaliwa ni vema ijielekeze katika kuhimiza matumizi bora ya rasilimali, uwekezaji katika nishati mbadala na teknolojia rahisi na nafuu, na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira.

Kuhusu biashara ya kaboni, Makamu wa Rais amesema ni muhimu kuwepo kwa uratibu madhubuti katika utekelezaji wa biashara ya kaboni kwa kuwa biashara hiyo inahusisha wadau wengi, hivyo ni muhimu kukutana kwa ajili ya kujadili na kupata mwelekeo wa pamoja katika uendeshaji wa biashara hiyo.

Pia Makamu wa Rais alisema ni muhimu kupata uzoefu kuhusu uendeshaji wa biashara ya kaboni kutoka nchi nyingine ili kuona namna zinavyokabiliana na changamoto zinazojitokeza.

Ameeleza kuwa uwazi katika mikataba ya biashara ya kaboni utasaidia uendeshaji wa biashara hiyo na kuondoa hali ya kutoaminiana. Amesema kwa sehemu kubwa, uendeshaji wa biashara hiyo umetawaliwa na madalali ambao pia utaratibu wa upatikanaji wao hauko wazi.

Mhe. Dkt. Mpango amesisitiza kuwa taratibu za jinsi biashara ya kaboni inavyofanyika zinapaswa kuwekwa wazi kwa wadau wakuu yaani wanavijiji na halmashauri ambao ndiyo wamiliki wa misitu na kuviagiza vyombo vya habari na taasisi za teknolojia kuongeza jitihada katika kutoa elimu ya biashara ya kaboni.





Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Joyce Mnunguli kuhusu Mfumo Jumuishi wa Taifa wa Usimamizi wa Mazingira (E-Mazingira) wakati akikagua mabanda ya maonesho katika Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akishuhudia gari la usafi linalotumia umeme ili kulinda mazingira linalomilikiwa na Kampuni ya Suma JKT wakati akikagua mabanda katika Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.







Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akizindua Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Taarifa za Mazingira nchini wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika Kitaifa jijini Dodoma.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akikabidhiwa zawadi ya Tuzo ya Mazingira kwa kutambua mchango wake katika uhifadhi mazingira wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. Anayekabidhi tuzo hiyo ni Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis.





# MAKAMU WA RAIS AONGOZA KIKAO KUJADILI MUUNGANO



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango ameongoza Kikao cha Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ya kushughulikia masuala ya Muungano kilichofanyika Ikulu, Dar es Salaam tarehe 04 Aprili 2025.

Katika kikao hicho, masuala mbalimbali yanayohusu Muungano yamejadiliwa kwa lengo la kutatua hoja mbalimbali na kuimarisha zaidi Muungano.

Kikao hicho kimehudhuriwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, Naibu Waziri Mkuu, Mhe. Dotto Biteko, Waziri Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhandisi Hamad Masauni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi) Mhe. Hamza Hassan Juma.

Pia, mawaziri na naibu mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Katibu Mkuu Kiongozi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Balozi Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhandisi Zena Said, makatibu wakuu, wakuu wa taasisi na wataalamu mbalimbali.





> “Kujenga Uchumi wa Buluu Imara katika Mkondo wa Bahari wa Pemba: Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Bahari kwa Maisha Endelevu na Mabadiliko ya Tabianchi




# DKT. MPANGO AHIMIZA USIMAMIZI IKOLOJIA BAHARI

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amesema Tanzania imedhamiria kuhakikisha usimamizi wa mkondo wa Pemba pamoja na ikolojia ya baharini kwa ujumla unakuwa endelevu.

Makamu wa Rais amesema hayo wakati akifungua Mkutano wa pembezoni uliohusu “Kujenga Uchumi wa Buluu Imara katika Mkondo wa Bahari wa Pemba: Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Bahari kwa Maisha Endelevu na Mabadiliko ya Tabianchi” uliofanyika kando ya Mkutano wa Tatu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Bahari uliofanyika jijini Nice nchini Ufaransa Juni 10, 2025.

Amesema dhamira ya nchi ni kuhakikisha Uchumi wa Buluu unakuwa kielelezo cha ukuaji jumuishi, utunzaji wa mazingira na ustahimilivu wa muda mrefu na kusisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa pamoja katika kuchukua hatua za haraka ili kulinda bahari kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.



Makamu wa Rais ameeleza kuwa Tanzania inachukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na hatari zinazoikumba ikolojia ya bahari ili kuhakikisha mkondo wa Pemba unakuwa himilivu pamoja na uendelevu wa mazingira kwa muda mrefu.

Alitaja hatua hizo kuwa ni pamoja na kuimarisha uhifadhi wa bahari kupitia Usimamizi imara na Uongezwaji wa Maeneo ya Hifadhi ya Bahari (MPAs), ambapo ametaja maeneo mawili mapya ya uhifadhi kisiwani Pemba yako katika hatua za mwisho za kutangazwa, hivyo kuimarisha azma ya nchi ya kulinda urithi wa kipekee wa bahari.

Pia, Mhe. Dkt. Mpango alisema Tanzania inahakikisha ushiriki wa jamii katika uhifadhi wa bahari kwa maendeleo ya Uchumi wa Buluu unaohusisha ufanyaji kazi kwa pamoja ili kuhakikisha juhudi za maendeleo ya baharini na pwani ni jumuishi, zenye usawa na endelevu.

Alitaja hatua nyingine kuwa ni kusaidia njia mbadala za maisha, kuimarisha minyororo ya thamani kwa wavuvi wadogo na kufungua fursa za ustawi kwa jamii za pwani sambamba na kuhifadhi mfumo wa ikolojia.

Mkondo wa Pemba ni eneo linalopatikana kati ya Tanzania Bara Mkoa wa Tanga na Kisiwa cha Pemba, Zanzibar hivyo ni eneo lenye ikolojia muhimu katika sekta ya bahari linalojumuisha miamba ya matumbawe, nyasi za bahari na mifumo ya ikolojia ya mikoko ambayo inachagiza sekta ya uvuvi nchini na kusaidia jamii za pwani na hutumika kama kinga dhidi ya athari zinazoongezeka kutokana na mabadiliko ya tabianchi.



# MAKAMU WA RAIS ATAKA TAFITI UBORA WA MAJI

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango amesema tafiti zinahitajika zaidi katika menejimenti ya rasilimalimaji ili kuwezesha maarifa mapya na uelewa mpana kuhusu upatikanaji na ubora wa maji.

Makamu wa Rais amesema hayo wakati akifungua Kongamano la Nne la Kimataifa la Kisayansi la Maji lililofanyika katika Ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam Januari 29, 2025.

Alisema ni muhimu tafiti kuelekezwa kujibu changamoto zinazokabili menejimenti ya rasilimali za maji hususani kubaini, kuotesha na kutunza miti ya asili ambayo inafahamika katika maeneo mbalimbali ya kila wilaya au mikoa nchini kuwa ni rafiki wa maji.

Mhe. Dkt. Mpango alisisitiza umuhimu wa tafiti hizo kuangazia teknolojia rahisi, endelevu na ya gharama nafuu ya kuvuna maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, sambamba na uchimbaji wa mabwawa, na kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua.

Aidha, Makamu wa Rais alitoa rai kwa kongamano hilo kuangazia suala la kubuni mikakati ya kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama na huduma za uondoshaji majitaka kwa wote na kutoa kipaumbele kwa jamii zilizo katika mazingira hatarishi.

Alisema suala hilo linapaswa kuhakikisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi yanajumuishwa katika mipango ya kila nchi ili kuendeleza matumizi bora ya maji na mifumo ya uondoaji wa majitaka pamoja na kujenga uwezo wa jamii kutambua, kuhimili na kukabiliana na matukio ya hali mbaya ya hewa.







Makamu wa Rais alisema Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuweka mazingira wezeshi yatakayorahisisha ushirikiano katika uendelezaji wa rasilimalimaji. Aidha, amewaalika watafiti na wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kushirikiana na Serikali katika menejimenti ya rasilimalimaji.

Kwa upande wake, Waziri wa Maji, Jumaa Aweso alisema Chuo cha Maji kimeendelea kuwa sehemu muhimu ya maendeleo ya sekta ya maji nchini kupitia ufundishaji na uendelezaji wa wataalamu wa maji nchini pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu ikiwamo kufanya tafiti mbalimbali ili kuondoa changamoto zinazoikabili sekta hiyo.




> “Muhimu tafiti kuelekezwa kujibu changamoto zinazokabili menejimenti ya rasilimali za maji hususani kubaini, kuotesha na kutunza miti ya asili ambayo inafahamika katika maeneo mbalimbali ya kila wilaya au mikoa nchini kuwa ni rafiki wa maji.
>
> **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango**
> Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania




# BIASHARA YA KABONI: WAWEKEZAJI WAFUNGULIWA MILANGO

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Japan zimetia saini Hati ya Makubaliano ya ushirikiano katika mpango wa pamoja wa uwekezaji katika biashara ya kaboni utakaowezesha kampuni za nchi hizo mbili kuwekeza katika biashara hiyo nchini Tanzania.

Utiaji saini wa makubaliano hayo umefanyika Mei 28, 2025 Tokyo, Japan kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni na Serikali ya Japan ikiongozwa na Waziri wa Mazingira, Mhe. Asao Keiichiro (Kei).

Akizungumza baada ya utiaji saini huo, Waziri Masauni amesema Makubaliano ya Ushirikiano yaliyosainiwa yamekusudia kuimarisha uhusiano kati ya Japan na Tanzania kwa maendeleo endelevu na hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Amesema ushirikano huo utaongeza fursa ya kupanua soko la biashara ya kaboni kutoka kwa wawekezaji wa Japan watakaowekeza katika miradi ya biashara hiyo itakayoibuliwa nchini.



Waziri Masauni ameeleza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anawataka wataalamu kutoka nchi hizi mbili kufanya kazi haraka, kwa bidii na kwa pamoja kwa manufaa ya nchi zote mbili ili kuhakikisha kuwa makubaliano hayo yanakwenda katika hatua ya utekelezaji.

"Tuko tayari kufanya kazi kwa ukaribu na wenzetu wa Japan ili kuhakikisha makubaliano haya yanatekelezwa kwa faida ya nchi zote mbili. Tayari Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeimarisha uwezo wa kitaasisi na kisheria katika usimamizi wa biashara ya kaboni ambapo Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa Kanuni za Mwaka 2022 za kuratibu biashara ya kaboni," alisisitiza Mhe. Masauni.

Aidha, Mhandisi Masauni alibainisha kuwa katika Mfumo wa Kitaasisi, Serikali imeanzisha Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni (NCMC) kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2025.
Hafla ya utiaji saini ilihudhuriwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhandisi Cyprian Luhemeja na watendaji kutoka ofisi hiyo.

> Tuko tayari kufanya kazi kwa ukaribu na wenzetu wa Japan ili kuhakikisha makubaliano haya yanatekelezwa kwa faida ya nchi zote mbili
>
> Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni
> Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)

# MFUMO WA KURATIBU **MUUNGANO** WAANZISHWA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni amelieleza Bunge kuwa katika mwaka 2024/2025 Serikali imeanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Kuratibu masuala ya Muungano na Yasiyo ya Muungano **(UNUMMiS).**

Akiwasilisha Hotuba ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka 2025/2026, Waziri Masauni amesema mfumo huo umelenga kurahisisha upatikanaji wa taarifa na utendaji kazi

Waziri Masuani alisema mfumo huo kwa sasa upo katika hatua za majaribio ili kuona kama unakidhi matakwa ya watumiaji na pindi utakapokamilika utasaidia wananchi kufahamu kwa kina masuala muhimu yanayohusu Muungano.

Aidha, Mhe. Masauni alisema Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu masuala ya ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuhakikisha wizara/idara na taasisi zinafanya vikao vya ushirikiano.

Ameongeza kuwa hadi kufikia Machi 2025 jumla ya vikao vinane vya ushirikiano vilifanyika vilivyolenga katika kubadilishana uzoefu, sera, sheria na utaalamu katika utekelezaji wa mambo yasiyo ya Muungano.

Mhandisi Masauni alisema katika kuimarisha sekta ya hifadhi na usimamizi wa mazingira nchini, Serikali kupitia Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni imesajili jumla ya miradi 73 ya biashara ya kaboni ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.


Aliongeza kuwa biashara ya kaboni imeanza kuleta manufaa kiasi katika baadhi ya maeneo nchini, ambako kiasi cha Shilingi bilioni 45 zimelipwa na kunufaisha wananchi katika halmashauri 10 nchini kama gawio la mauzo ya viwango vya kaboni.

**"Ofisi iliratibu vikao mbalimbali ikiwa ni pamoja na kikao cha kuwajengea uwezo makatibu wakuu 21 kuhusu biashara ya kaboni, wawakilishi wa makampuni 27 yanayojihusisha na biashara ya kaboni, vikao vya kimkakati vya kuimarisha usimamizi wa biashara ya kaboni baina ya Ofisi ya Makamu wa Rais na wizara za kisekta,"** alisema **Waziri Masauni.**

Kuhusu uchumi wa buluu, Waziri Masauni alisema Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ikiwamo kuandaa Mpango wa Matumizi wa Maeneo ya Maji pamoja na kuwezesha uwepo wa utafiti na ujuzi katika matumizi ya rasilimali za uchumi wa buluu nchini.

Kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Sura 191, Mhandisi Masauni alisema hadi kufikia Machi 2025, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), lilipokea na kushughulikia malalamiko 247 yaliyohusu kelele, utupaji taka ovyo, utiririshaji ovyo wa majitaka, ujenzi holela, uchimbaji usio rasmi wa mchanga na uchafuzi wa hewa.

Bunge lilidhinisha kiasi cha **shilingi bilioni 81,864,190,000** kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2025/2026 ambayo tayari utekelezaji wake umeanza.






# Waziri Masauni
## Azindua mradi wa utunzaji wa vyanzo vya maji

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Mhandisi Hamad Yusuf Masauni amezindua Mradi wa Suluhisha 'Resolve' unaolenga katika utunzaji wa vyanzo vya maji, misitu na maeneo yanayohusika na shughuli za kilimo.**

**Mradi huo unaotekelezwa na Shirika la Kimataifa la Hifadhi ya Mazingira, utatekelezwa katika mikoa ya Morogoro na Iringa kwa miaka mitatu.**

Sanjari na kuzindua mradi huo, Waziri Masauni amefunga warsha ya wadau wanaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD) linalohusu uhusiano uliopo baina ya mabadiliko ya tabianchi na kilimo.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, amesema Ofisi ya Makamu wa Rais itaendeleza dhamira yake ya kuunga mkono sera na programu zinazokuza kilimo endelevu na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Pia, Waziri Masauni amesema ofisi yake itaendelea kufanya kazi kwa karibu na wadau wote ili kukusanya rasilimali, kuimarisha uwezo na kuleta mabadiliko yenye matokeo na kufanikiwa kwa miradi iliyopo na mipya itakayoonesha dhamira katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

"Kwanza kabisa, nitoe shukrani zangu za dhati kwa washiriki wote, watafiti wetu, watendaji wetu, watunga sera, wakulima na washirika wa maendeleo kwa ushiriki wenu, michango ya busara na kujitolea katika kuandaa warsha hii muhimu ya kilimo na mabadiliko ya tabianchi," alisema Mhandisi Masauni.

**"Kilimo kinasalia kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania, kinatoa riziki kwa watu wengi na kuchangia kwa kiasi kikubwa usalama wa chakula wa taifa na ukuaji wa uchumi. Hata hivyo, tunafahamu kikamilifu kwamba sekta hii muhimu iko hatarini zaidi kwa athari za mabadiliko ya tabianchi,"** aliongeza.

Aidha, Mhe. Masauni amesema kupanda kwa halijoto, mvua zisizo na mpangilio, ukame wa muda mrefu, na matukio mengine mabaya ya hali ya hewa huleta tishio kubwa kwa tija ya kilimo, mifumo ikolojia na maisha ya vijijini.



Kwa upande wake, Mratibu wa mradi huo, Bw. Anthony Mhagama amesema mradi umefika wakati muhimu ambao Tanzania kama nchi nyingine imekuwa ikikabiliwa na mabadiliko ya tabianchi hivyo utasaidia jamii kupata mbinu za kukabiliana na changamoto mbalimbali za mabadiliko ya tabianchi.

Warsha hiyo imeangazia mambo kadhaa muhimu ya kuchukua kama vile haja ya dharura ya kujumuisha mbinu za kilimo zinazozingatia mabadiliko ya tabianchi ili kuongeza tija huku kupunguza utoaji wa gesi chafuzi.

Pia wataalamu hao waliangalia umuhimu wa kuendeleza utafiti, uvumbuzi, na uhamisho wa teknolojia ili kuwawezesha wakulima kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa pamoja na umuhimu wa uwiano wa sera na ushirikiano katika sekta zote ili kufikia malengo yetu ya pamoja.



# NISHATI SAFI YA KUPIKIA;
## MATUMIZI YAHIMIZWA

**Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Khamis Hamza Khamis amehimiza wananchi kuendelea kuunga mkono Serikali katika kutumia nishati safi ya kupikia ambayo ni rafiki kwa mazingira.**

Ametoa kauli hiyo wakati akitembelea na kukagua mabanda ya maonesho ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani Juni 4, 2025 kwenye Viwanja vya Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Mhe. Khamis alisema matumizi ya nishati safi ya kupikia sio gesi pekee kama ambavyo wengi wanafikiria, bali inajumuisha nyenzo zote za kupikia ambazo haziharibu mazingira zikiwamo mkaa mbadala na majiko janja yanayoitumia kiwango kidogo cha umeme.

Alisema Serikali imetatua changamoto ya umeme kwa kutekeleza Mradi wa Kufua Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) na kusambaza nishati hiyo vijijini ili kuwezesha wananchi wengi kunufaika nayo kwa bei nafuu.
Aidha, alipongeza Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuendelea kufunga miundombinu ya gesi katika kambi zao na hivyo kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Akiendelea kutembelea mabanda ya wizara, taasisi na kuzungumza na wadau wa mazingira, aliwapongeza kwa juhudi zao za kushirikiana na Serikali katika kusukuma mbele ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Katika hatua nyingine, aliwapongeza wadau kwa kubuni mbinu mbalimbali za kusimamia taka zikiwamo kurejeleza taka kwa kuzalisha bidhaa mbalimbali zikiwamo mbolea.
Mhe. Khamis alisema hatua hiyo ni mojawapo ya uungaji mkono Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka (2025-2030) uliozinduliwa na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa.






> Katika hatua nyingine, aliwapongeza wadau kwa kubuni mbinu mbalimbali za kusimamia taka zikiwamo kurejeleza taka kwa kuzalisha bidhaa mbalimbali zikiwamo mbolea.
>
> Mhe. Khamis Hamza Khamis
> Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)



# MAPAMBANO UKAME NA JANGWA; WADAU WAITWA

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Khamis Hamza Khamis ametoa rai kwa wadau wa mazingira katika ngazi zote na wananchi kwa ujumla kuungana na Serikali kwa hali na mali katika mapambano dhidi ya kuenea kwa hali ya jangwa na ukame kwa faida ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

Pia, amewaomba wananchi kuendelea kupanda miti na kuitunza ili kukabiliana na athari za ukame ambao unaathiri sekta mbalimbali ikiwemo maji, mifugo na kilimo ambazo zina umuhimu mkubwa kwa binadamu.

Ametoa wito huo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Umoja wa Mataifa ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame Duniani yaliyofanyika kitaifa Juni 17, 2025 katika Manispaa ya Shinyanga.

Akizungumza na viongozi na wananchi, Mhe. Khamis amesema pamoja na mambo mbalimbali, Tanzania pamoja na jumuiya za kimataifa kwa kushirikisha vizazi vilivyopo na vijavyo, imejitolea kuongoa hekta bilioni moja ya ardhi iliyoharibika kufikia mwaka 2030.

Alisema Tanzania ni moja ya waathirika wa hali ya ukame hivyo Serikali imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha inakabiliana na tatizo hilo kwa ufanisi mkubwa kwa kushirikisha wizara za kisekta, taasisi za umma, washiriki wa maendeleo, mashirika yasiyo ya kiserikali, sekta binafsi na taasisi za kidini.

Halikadhalika, Naibu Waziri Khamis alibainisha kuwa Serikali imeandaa Mpango wa Kitaifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame na imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mazingira.



Akizungumzia siku hiyo, alisema ina madhumuni ya kukuza uelewa miongoni mwa jamii juu ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame na umuhimu wa utekelezaji wake duniani kote, hususan katika nchi zilizoathirika zaidi hasa Afrika.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Mhe. Julius Mtatiro aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa aliishukuru Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuona umuhimu wa kuadhimisha siku hii mkoani humo.

Alisema kutokana na mkoa huo kukabiliwa na hali ya ukame hivyo ni jambo jema kuitumia siku hiyo kuhamasisha upandaji wa miti kuepuka changamoto ya kugeuka kuwa jangwa.

Mhe. Mtatiro aliishukuru Serikali chini ya Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wananchi ambayo si tu inasaidia katika utunzaji wa mazingira, bali pia inachagiza uchumi.

# JNHPP; KITOVU CHA NISHATI SAFI YA KUPIKIA





Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis amesema Mradi wa kufua Umeme wa Bwawa wa Julius Nyerere uliopo Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2115 utachochea matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Amesema hayo wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Donge Mhe. Soud Mohammed Jumah aliyetaka kufahamu ni kwa kiasi gani mradi huo umechangia matumizi ya nishati safi ya kupikia na kuepuka ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

Akiendelea kujibu swali hilo Naibu Waziri Khamis amesema tayari Serikali imesambaza huduma ya umeme wa uhakika mijini na vijijini hatua itakachagiza matumizi ya nishati safi ya umeme na kuacha kutumia kuni na mkaa.

Aidha, Mhe. Khamis alisema katika kuimarisha uhifadhi wa mazingira hususan katika maeneo yanayozunguka mradi huo wa kufua umeme, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kuhamasisha na kuratibu upandaji wa miti kwenye vyanzo vya maji na kuitunza.

Alisema Serikali imeendelea kutoa elimu ya mazingira, kusimamia utekelezaji wa Muongozo wa Taifa wa Matumizi endelevu ya Ardhi Eneo la Hifadhi ya Mita Sitini kutoka kwenye vyanzo vya maji pamoja na kuunda Kamati za Mazingira kwa ajili ya kudhibiti uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo vya maji.

Alisema hayo wakati akijibu swali la msingi la Mhe. Soud aliyeuliza kuna mkakati gani wa kuimarisha uhifadhi wa mazingira ya Mradi wa Bwawa la Nyerere ili kuhakikisha uendelevu wa mradi.

“Ushirikishwa wa wananchi waishio karibu na mradi huo unafanyika wa kiasi kikubwa na tumewapa jukumu la kutunza mradi na pia tunawahimiza kupanda miti ambayo haikaushi maji, vilevile tunashirikiana na maafisa wa mazingira na mabalozi wa mazingira, lakini pia tunawahamisha mara kwa mara wafanye usafi ili eneo la bwawa liendelee kuwa safi,“ alisema.

Kwa upande mwingine, alisema Serikali itaendelea kuwachukulia hatua wanaojihusisha na vitendo vya ukataji miti hususan maeneo yanayozunguka miradi mikubwa na vivutio vya utalii hususan Mlima Kilimanjaro.

Alitoa kauli hiyo wakati akijibu swali la Mbunge wa Moshi Vijijini Prof. Patrick Ndakidemi kuhusu hatua gani Serikali inawachukulia hatua wanaokata miti katika hifadhi ya Mlima Kilimanjaro.
Mradi wa Bwawa la Nyerere unalenga kufikia malengo ya Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034) kuwa asilimia 80 ya Watanzania kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Hivyo, hizo ni juhudi za Serikali chini ya Rais Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amewa kinara katika kuhamasisha jamii kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia.

# Mradi wa Urejeshaji wa **Mazingira** kuongezewa wigo

**Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhandisi Cyprian Luhemeja amesema ofisi hiyo imekusudia kuongeza wigo wa maeneo ya utekelezaji wa Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bayoanuai Tanzania (SLR-Tanzania) ikihusisha Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji.**



Mhandisi Luhemeja amesema hayo Machi 15, 2025 Jijini Mbeya wakati akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kumalizika kwa kikao cha kamati tendaji ya kitaifa ya usimamizi wa mradi huo kilichojadili shughuli za utekelezaji wa mradi hadi kufikia sasa.

Luhemeja amesema tathimini iliyofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais katika Mikoa na Halmashauri zinazotekeleza mradi huo, imeonesha wananchi wengi wamefurahishwa na utekelezaji wa shughuli za mradi na hivyo Serikali imepanga kuhakikisha kuwa inaongeza wigo wa maeneo ya utekelezaji wake.

“Mwezi Oktoba mwaka huu tutafanya tathimini ya mradi na ili kuona uwezekano kupata maeneo mengi zaidi ya utekelezaji na kuwanufaisha wananchi kwani wengi wao wamevutiwa na fursa zitokanazo na uhifadhi endelevu wa mazingira kupitia shughuli mbadala za kiuchumi” amesema Luhemeja.

Ameongeza kuwa kupitia mradi wa SLR Serikali, imepanga kubuni miradi mingi zaidi ya kijamii na kiuchumi kwa ajili ya kusaidia jamii na hivyo kuongeza hamasa kwa jamii kutumia vyema fursa ya mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuibua fursa mbalimbali.

Amefafanua kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kujenga uwezo kwa jamii zinazotekeleza mradi huo ziweze kuhamasisha katika masuala ya uhifadhi wa mazingira na kutumia fursa zilizopo kuweza kujiongeza kipato kupitia shughuli za uzalishaji mali.

“Tumeona Mkoa wa Katavi na Wilaya ya Mpimbwe wananchi wamehamasika kupanda miti na kuingia katika biashara ya kaboni na hivyo kujiongeza kipato.....Tumejipanga kuhakikisha fursa hizi pia zinaweza kuwanufaisha wananchi wa maeneo mbalimbali nchini” amesema Mhandisi Luhemeja. Ameeleza kuwa kupitia mradi wa SLR wananchi wameweza kutumia mbinu za kisasa za uzalishaji mali ikiwemo kilimo rafiki kwa mazingira ambacho kimewazesha wananchi kuweza kuvuna kiasi kikubwa cha mazao na kujiwekea akiba kwa kutumia mbinu za kisasa ikiwemo mbegu bora na teknolojia ya umwagiliaji.

Aidha Luhemeja amezihimza jamii zilizonufaika na mradi huo kutumia vyema rasilimali zilizopo ili kuwa endelevu sambamba na kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha jamii kutunza na kuhifadhi mazingira kwani Serikali itaendelea kutafuta fedha za kuwezesha miradi mbalimbali ya mazingira.

Kwa upande wake Mratibu wa Kitaifa wa Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bayoanuai Tanzania (SLR), Dkt. Damas Mapunda amesema mradi huo umekuwa mkombozi kwa jamii zilizoathirika na uhalibifu wa mazingira kwa kuwapatia shughuli mbadala kwa ajili ya uzalishaji mali.

“Mradi huo umepata ushirikiano mkubwa katika utekelezaji wake kutoka katika sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa, hatua inayowezesha Serikali kuweza kufikia malengo iliyojiwekea ya urejeshwaji wa uoto wa asili katika maeneo mbalimbali nchini” amesema Dkt. Mapunda .

Ameongeza kuwa hadi kufikia sasa mradi huo umefikia asilimia 67 ya utekelezaji wake na kuongeza kuwa Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wote ili kukamilisha mradi huo kwa kwa wakati na viwango vilivyokusudiwa.

Mradi wa SLR unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) kupitia Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP) na kusimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais ambapo kiasi cha Bilioni 25.8 kimetengwa kwa ajili ya utekelezaji. Mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2021 na unatarajia kukamilika mwaka 2025 na ambapo jumla ya Mikoa 5,

Halmashauri 7, Kata 18 na vijiji 54 zinatarajia kunufaika. Halmashauri hizo ni Iringa Vijijini, Mbeya, Mbarali, Sumbawanga Vijijini, Tanganyika na Mpimbwe.




# **KUIMARISHA MUUNGANO;** KAMATI YA PAMOJA YAKUTANA

Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imekutana kujadili masuala ya Muungano jijini Dar es Salaam tarehe 21 Februari 2025.

Kikao hicho kimeongozwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhandisi Cyprian Luhemeja pamoja na Mwenyekiti Mwenza ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Bw. Islam Seif Salum.

Aidha, kikao hicho pia kimehudhuriwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu (SMZ), Bw. Saleh Juma Mussa, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (SMZ), Bi. Mansura Mosi Kassim na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dkt. Jim Yonazi.

Wengine ni Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria (SJMT), Bi. Angela Anatory, Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais, Bw. Abdallah Hassan Mitawi, Mkurugenzi wa Muungano Ofisi ya Makamu wa Rais, Dkt. Juma Mohamed Salum ambaye pia ni Katibu wa kikao na Mkurugenzi wa Uratibu na Shughuli za Serikali Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Bi. Siajabu Suleiman Pandu (Katibu Mwenza) pamoja na wataalamu kutoka SJMT na SMZ.

Kikao cha Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ hufanyika kwa mzunguko katika kila upande wa Muungano kujadili masuala ya Muungano.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA MAKAMU WA RAIS

**JARIDA HILI LIMETOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**Ofisi ya Makamu wa Rais**

Barua pepe: **ps@vpo.go.tz**

**blog.vpo.go.tz**



**www.vpo.go.tz**